

**Maelekezo ya Kufika Chuoni**

Chuo kipo KM 5 kutoka Morogoro Mjini au KM 8 kutoka stendi ya mabasi Msamvu uelekeo wa njia ya zamani ya DSM (old DSM road) kuelekea Bigwa na kipo kandokando ya Milima Uluguru.

**Hali ya Hewa**

Chuo kipo mazingira mazuri kandokando ya Mlima. Hali ya hewa ya hapa chuoni ni ile ya "Coastal mountainous" na hali ya joto ni kuanzia nyuzi joto 19°C hadi 30°C. Kipindi cha mvua ni kuanzia mwezi Februari hadi Mei.

**Masomo yanayofundishwa**

Chuo hiki cha Morogoro kinachukua wanachuo wa Stashahada ya Kawaida miaka Miwili na Stashahada Maalumu ya miaka Mitatu ya Ualimu, Elimu ya Msingi.

**Motto wa Chuo**

WATU WAPASWA KUFAHAMU

# KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU MOROGORO





**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

## CHUO CHA UALIMU MOROGORO

**S.L.P 691, MOROGORO**

SIMU: +255 260 3867 Au +255786 647323 Au +255713620350

E-Mail: morogorotc@gmail.com
morogorotc@moe.go.tz
Website: www.morogorotc.ac.tz

WATU WAPASWA KUFAHAMU

# FOMU YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA MAALUM YA UALIMU, ELIMU YA MSINGI MWAKA 2025/2026

**Ndugu, ……………………………………………..**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA KAWAIDA NA MAALAMU YA UALIMU WA SHULE YA MSINGI SAYANSI, HISABATI NA TEHAMA 2025/2026**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Chuo hiki kwa mafunzo ya Stashahada ya Kawaida/Maalumu ya Ualimu Elimu ya msingi.

**1.2 MAAGIZO YA JUMLA.**

Ili uweze kusajiliwa unatakiwa kuzingatia yafuatayo:

a) Uwe na vyeti halisi (Original Certificates) vilivyotolewa na BARAZA LA MITIHANI tu, pamoja na nakala zake (photocopies) za kidato cha nne (CSEE) kwa Stashahada Maalumu na (ACSEE) kwa Stashahada ya Kawaida pamoja na vyeti vya kuhitimu (leaving certificates).

b) Uwe na barua ya kujiunga na Chuo iliyosainiwa na Mkuu wa Chuo.

c) (Fomu ya afya ilichosainiwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali-Fomu imeambatishwa.

d) Rimu moja ya karatasi A4 (SMART COPY au Aone photocopy paper)

e) Lazima kila mwanachuo kuwa na **BIMA YA AFYA.** Kama hana atatakiwa kuchangia **shs 50,400/=** kwa ajili ya kupatiwa kitambulisho cha bima ya afya **(NHIF).** Mwanachuo hatopokelewa bila Kitambulisho hicho.

f) Kila mwanachuo atatakiwa kuwa na **Mihtasari (syllabi) mbili** za masomo ya mchepuo shule ya msingi (Stashahada miaka 2) na angalau kitabu kimoja cha A-level katika kila somo kwa stashahada miaka 3 (Vitabu viwe vya Taasisi ya Elimu Tanzania).

**1.3 MAAGIZO YANAYOHUSU FEDHA**

**1.3.1 Ada**

a) Ada ya Mafunzo ni Sh. **450,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa nusu **225,000/=** kwa muhula.

**1.3.2 Michango**

a) Mchango wa Usajili na kitambulisho Tshs. 20,000/= Mwaka wa kwanza tu

b) Mchango wa huduma ya kwanza Tsh10,000/= kwa mwaka

c) Serikali ya wanachuo Tshs. 5,000/= kwa mwaka

d) Ulinzi Tshs. 30,000/= kwa mwaka

e) Ukarabati TShs. 25,000/= kwa mwaka.

f) Michezo Tshs. 30,000/= Kwa mwaka.

g) Vifaa vya Usafi TShs. 20,000 kwa mwaka

h) Kukodi godoro TShs. 10,000/= kwa mwaka.

**Jumla ya michango yote ni TShs. 150,000/= kwa Mwaka**

**ADA YA CHUO INALIPWA KWA KUTUMIA CONTROL NUMBER. WASILIANA NA MHASIBU WA CHUO KWA NAMBA 0717013226 KUPATA CONTROL NUMBER YA KULIPA ADA.**

**MICHANGO YOTE ILIPWE CRDB**: Jina la Akaunti - **Morogoro Teachers' College. Akaunti No. 01J1076984900.**

Uje na Stakabadhi ya malipo (Original). Usisahau kuandika jina lako nyuma ya Stakabadhi unapoweka fedha benki.

**NB: MWANACHUO ASIYEKAMILISHA MALIPO YA ADA NA MICHANGO HATAPOKELEWA CHUONI.**

**1.4 SARE YA CHUO.**

**Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na sare kama ifuatavyo.**

**(i ) WANAWAKE:**

- Mashati mawili mikono mirefu-Light Blue
- Suti nyeusi mbili za heshima (angalia mchoro wa Sketi ulioambatishwa)
- Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi
- Tai mbili nyeusi fupi
- Koti jeupe la Maabara (Wanaosoma Physics, Chemistry na Biology)
- Kwa Waislam-Hijab rangi ya light blue
- Soksi nyeusi

**(ii) WANAUME:**

- Mashati mawili mikono mirefu – Light Blue
- Suti nyeusi mbili za heshima (Angalia mchoro wa Suruali ulioambatishwa). Koti vifungo viwili
- Viatu vyeusi vya ngozi
- Tai mbili nyeusi ndefu.
- Koti jeupe la Maabara (Wanaosoma Physics, Chemistry na Biology)
- Soksi nyeusi

**1.5 MAHITAJI MENGINE**

a) Uje na blanketi, shuka mbili za pinki au light blue, mto na foronya, pia chandarua.

b) Daftari (counter book) kumi (10), mathematical seti, na Calculator

c) Vyombo vya chakula kama Sahani na Kikombe

**1.6 VIFAA VYA MICHEZO**

a) Tracksuit ya Bluu bahari na T-shirt nyeupe (Chuoni zinapatikana kwa Tshs. 20,000/=)

b) T-Shirt itanunuliwa Chuoni. Uje na Tsh. 15,000/=

c) Raba nyeusi za michezo na soksi zake

d) Jezi ya rangi ya blue au nyeupe moja.

**1.7 KUWASILI CHUONI.**

Unatakiwa kufika Chuoni tarehe **18/08/2025.** Mwisho wa kuripoti Chuoni ni tarehe **30/08/2025.**

Unashauriwa kukodi tax ili ufike salama Chuoni. Hii ni kwa sababu Chuo kipo umbali wa Km. 8 kutoka kituo cha mabasi MSAMVU. Gharama ya kukodi Tax wastani ni sh.10,000/= hadi 15,000/= toka MSAMVU hadi CHUONI. Kwa usalama wako ukifika usiku tafadhali chukua Taxi ndani ya kituo cha mabasi siyo nje ya kituo.

**1.8 MAMBO MUHIMU UKIFIKA CHUONI.**

Ufikapo Chuoni pitia hatua zote za kusajiliwa kama ifuatavyo:

a) Jiandikishe ufikapo lango kuu

b) Fika ofisi ya Udahili na uoneshe vyeti kama ulivyoagizwa. Rejea No.1.2 na stakabadhi za malipo ulizolipia ada na michango.

c) Ofisi akithibitisha kuwa umekamilisha maagizo yote muhimu atakudahili na kukukabidhi Ofisi ya Masuala ya Wanachuo ili upangiwe Bweni.

d) Huruhusiwi kwenda Bwenini bila kusajiliwa.

1.9 Maelekezo muhimu kuhusu mafunzo yako na taratibu za Chuo yatatolewa wakati wa maelekezo ya awali (orientation) ukifika chuoni.

1.10 Sheria za Chuo, utatakiwa kuzisoma na kuzielewa, na kisha kuzisaini mbele ya Mzazi/Mlezi kabla ya kuwasili Chuoni.

1.11 Vyeti vyako vitahakikiwa na jopo MAALUM. Kwa hiyo jiridhishe mwenyewe kuwa vyeti hivyo ni halisi na halali

**KARIBU SANA CHUONI MOROGORO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU MOROGORO
S. L. P 691, MOROGORO

**AUGUSTINE J. SAHILI**
**MKUU WA CHUO**

**Nakala:**

Mkurugenzi Msaidizi - Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 10,
**40479 DODOMA.**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**PART A**: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO: The Medical Officer,

………………………………………………
………………………………………………
………………………………………………

From: **The Principal,**
Morogoro Teachers' College,
P. O. Box 691,
**MOROGORO.**

**18/08/2025**

**Mr/Miss/Mrs**…………………………………………………………………………………… (Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time teacher training course. The examination should include the following categories (I – IV) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect.

Pregnancy (Category IV) will also render a girl ineligible for the course.

i) (a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy

ii) Neuroses
iii) Other serious diseases
iv) Pregnancy

---

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)
I have examined the above named and considered that he/she is physically and mentally fit/unfit for a full-time teacher training course.

a) Eye-sight ………………………………………………………………………………………
b) Hearing ………………………………………………………………………………………..
c) Limbs ………………………………………………………………………………………….
d) Venereal diseases………………………………………………………………………………
e) Leprosy ………………………………………………………………………………………..
f) Epilepsy………………………………………………………………………………………..
g) Neuroses ………………………………………………………………………………………
h) Other serious diseases ………………………………………………………………………..
i) Pregnancy ………………………………………………………………………………………

Date ………………………………… Signature ………………………………………..

Station ……………………………… Designation ………………………………………

Official stamp

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**CHUO CHA UALIMU MOROGORO**

**S.L.P 691, MOROGORO**

e-mail: **morogorotc@gmail.com;**

**morogorotc@moe.go.tz**

---

## SHERIA ZA CHUO

Sheria hizi ni mwongozo wa namna ya kuishi na kuenenda kwa wanachuo wote wa Chuo cha Ualimu Morogoro wawapo chuoni na nje ya chuo. Hivyo, ni lazima kwa mujibu wa sheria za chuo kila mwanachauo kupata nakala ya sheria za chuo. Aidha, mwanachuo anapaswa kuweka sahihi na kurudisha nakala ya sheria iliyosainiwa kwa Mratibu wa masuala ya Wanachuo.

### 1. UTII WA SHERIA ZA NCHI NA ALAMA ZA TAIFA

**a)** Mwanachuo atawajibika kutii na kuzifuata sheria za nchi

b) Mwanachuo atawajibika kuzitii alama za Taifa kama vile bendera ya Taifa, nembo ya Taifa na wimbo wa Taifa

c) kwa namna yoyote ile na katika mazingira yoyote yale, mwanachuo hataruhusiwi kufanya udanganyifu ikiwa ni pamoja na kughushi nyaraka za kiserikali, kielimu au kiofisi

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 1(a) hadi 1(c) atachukuliwa hatua kwa utaratibu uliowekwa na sheria za nchi au kuachishwa mafunzo***

### 2. HESHIMA NA UTII

**a)** Mwanachuo atawajibika kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu wenzake, wafanyakazi wa chuo cha Ualimu mororgoro na watu wengine anaokutana nao.

**b)** Mwanachuo atawajibika kutoa salamu kwa heshima kwa kuzingatia utamaduni na maadili ya kitanzania

**c)** Ni wajibu wa kila mwanachuo kuwa na lugha yenye hadhi ya taaluma ya ualimu na matendo yake yawe yanakuza heshima na utu wake.

d) Mwanachuo ana wajibu wa kuheshimu na kufuata RATIBA KUU ya chuo na shughuli zinazoambatana na ratiba

e) Mwanachuo atawajibika kutii kengele au ishara nyingine yoyote itakayomhitaji kufika mahali anapotakiwa

f) Ni sharti kwa kila mwanachuo kuwahi wakati wowote anapohitajika chuoni mfano: kuripoti chuoni, mkusanyiko maalumu, bwaloni, ukumbini, darasani, katika kazi za nje na mahali pengine

g) Mwanachuo haruhusiwi kujihamisha bweni au chumba alichopangiwa. Aidha, kwa namna yoyote ile mwanachuo haruhusiwi kulala bweni ambalo hakupangiwa

h) Mwanachuo haruhusiwi kufanya udanganyifu au upotoshaji wa taarifa ya aina yoyote kwa jambo lolote wakati wote wa mafunzo

i) Mwanachuo haruhusiwi kufanya biashara yoyote awapo chuoni

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 2(a) hadi 2(i) atafunguliwa mashtaka na kupewa adhabu ya papo kwa papo na kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21) au kuachishwa mafunzo***

## 3. MAHUSIANO

**a)** Mwanachuo wa kike haruhusiwi Kwenda kwenye bweni la wanaume na mwanachuo wa kiume haruhusiwi kwenda kwenye bweni la wanawake isipokuwa kwa idhini maalumu

**b)** Ni kosa kwa mwanachuo yeyote yule kuonyesha dalili ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi /kuishi kama mke na mume na mwanachuo mwenzake au mfanyakazi wa chuo cha ualimu Morogoro au mtu mwingine yoyote

**c)** Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kutembelewa na kumpokea mgeni siku za masomo. Mgeni wa dharura wa mwanachuo (atakayekuja chuoni siku za masomo) anapaswa aelekezwe kwenda ofisi ya mratibu wa masuala ya wanachuo au ofisi ya zamu

**d)** Hairuhusiwi kwa mwanachuo yeyote yule kumpeleka/kumkaribisha mgeni asiyekuwa mwanachuo bwenini

**e)** Mwanachuo haruhusiwi Kwenda nyumbani kwa mkufunzi au mfanyakazi yeyote bila ruhusa maalumu

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 3(a) had 3(g) atafunguliwa mashtaka na kupewa adhabu ya papo kwa papo na kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua.***

***Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21) au kuachishwa mafunzo***

## 4. USAFI, AFYA NA MAZINGIRA

**a)** Mwanachuo haruhusiwi kuwa na kucha ndefu, ndevu, kunyoa kipara na meno yasiyopigwa mswaki. Aidha mwanachuo haruhusiwi kupaka rangi za kucha au midomo, kutinda nyusi au kuweka nyusi bandia au kucha bandia

**b)** Wakati wote ndani na nje ya chuo, mwanachuo atatakiwa kuvaa mavazi yenye heshima na safi kulingana na mwongozo wa mavazi

**c)** Mwanachuo anawajibu wa kuweka matandiko yake na vitu vingine chumbani katika hali ya usafi na unadhifu

**d)** Mwanachuo anawajibu wa kufanya usafi wa maeneo, bweni, bwalo la chakula, madarasa, kumbi, vyoo pamoja na maeneo mengine nyakati za asubuhi na siku za mpango kazi.

**e)** Mwanachuo haruhusiwi kutumia vileo kama kuvuta sigara, bangi, kunywa pombe, kujihusisha na dawa za kulevya, ushoga, usagaji na mambo mengine yanayofanana na hayo

**f)** Wagonjwa wanawajibu wa Kwenda zahanati/hospitali kupata ushauri na matibabu. Ruhusa za mapumziko zahanati zitatolewa na mganga au muuguzi.

**NB**: Kabla ya kusajiliwa ni lazima mwanachuo awe na cheti cha daktari kutoka katika hospitali ya serikali kinachoonesha hali ya afya yake

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 4(a) hadi 4(f) atafunguliwa mashtaka na kupewa adhabu ya papo kwa papo na kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21) au kuachishwa mafunzo***

## 5. MAVAZI

**a)** Sare au mavazi rasmi ya chuo yatavaliwa wakati wote wa vipindi au mwanachuo anapotoka nje ya chuo. Sketi ya wanachuo itapaswa kuwa si pungufu ya inch 5 kuanzia kwenye magoti kushuka chini na wale wanachuo wa kiume upana wa suruali si chinimya inchi 10

**b)** Hairuhusiwi kwa mwanachuo kuvaa kaptula, malapa, nguo za mipasuo inayovuka magoti, suruali za kubana, sketi fupi na zakubana na kofia katika maeneo ya chuo.

**c)** Kila mwanachuo atapaswa kuwa na pea moja ya tracksuit ambayo ataivaa muda wa michezo.

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 5(a) hadi 5(c) atapewa adhabu ya onyo kali na kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi ambazo ni kufanya usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21) au kuachishwa mafunzo***

## 6. RUHUSA KWA WANACHUO

Ruhusa kwa mwanachuo yeyote Kwenda nje ya chuo muda wa masomo zitatolewa na mkufunzi wa zamu. Aidha ruhusa zote za kulala nje ya chuo zitatolewa na mkuu wa chuo kupitia ofisi ya masuala ya wanachuo. Hivyo ni marufuku kwa mwanachuo kuondoka chuoni au kusafiri kwa muda mfupi au mrefu pasipo ruhusa

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria namba (6) atapata adhabu ya onyo kali na kiongozi wa serikali ya wanachuo, mkufunzi ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21) au kuachishwa mafunzo***

## 7. UTORO

Ni kosa kwa mwanachuo kutokuhudhuria vipindi vya masomo darasani bila sababu yoyote ile ya msingi au kibali maalumu kutoka kwa uongozi. Aidha mwanachuo haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa muda wa vipindi vya darasani

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria namba (7) atapewa adhabu ya onyo kali, kufanya shughuli za kitaalumana na kiongozi wa serikali ya wanachuo, mkufunzi pia anaweza kupewa adhabu ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku kumi na nne (14) au kurudia mwaka wa mafunzo***

***Na endapo siku za utoro zitazidi tisini (90) basi mwanachuo huyo atakosa sifa ya kuendelea na masomo na atakuwa amejiachisha mafunzo rasmi***

## *8.* CHAKULA

*a)* Mwanachuo haruhusiwi kula chakula nje ya bwalo la chakula isipokuwa pale atapoelekezwa vinginevyo na uongozi

*b)* Ni kosa kwa mwanachuo kupiga kelele au kusababisha kelele zisizo za lazima awapo katika bwalo la chakula

*c)* Ni kosa kwa mwanachuo kupika au kuwa na vifaa vya kupikia bwenini au mahali pengine popote bila idhini maalumu kutoka kwa uongozi

*d)* Ni kosa kwa mwanachuo kuwa na Vifaa hatarishi kama kama jiko, heater, drier, sufuria, kisu na vingine vinavyofanana na hivyo

*e)* Ni marufuku kwa mwanachuo kumkaribisha mtu yeyote kula chakula cha chuo na vilevile hapaswi kuleta chakula kutoka nje ya chuo bila kibali maalumu

*f)* Ni kosa kwa wanachuo kuingia bwaloni na viatu vya wazi kama makobazi, yeboyebo, kandambili, kaptula, kanga, vesti, gauni ya kulalia, skafu, taulo, kofia na vitu vinavyofanana na hivyo

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 8(a) hadi 8(f) atapata adhabu ya onyo kali kutoka kwa kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi pia anaweza kufanya adhabu zingine mfano usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua au kulipa gharama za umeme. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21)***

## UTUNZAJI WA MALI YA CHUO

**a)** Hairuhusiwi kuhamishja samani za chuo cha ualimu mororgoro (viti, gododro, meza n.k) kutoka sehemu moja Kwenda sehemu nyingine bila ya kibali kutoka uongozi wa Chuo cha ualimu morogoro

**b)** Hairuhusiwi kwa mwanachuo kupoteza au kuharibu kifaa/mali ya chuo kwa uzembe au kwa kukusaidia ikiwa ni pamoja na kuandika au kuchora kuta bila ya kibali kutoka katika uongozi wa chuo

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 9(a) hadi 9(b) ataadhibiwa kwa onyo kali au karipio kwa mara ya kwanza na kulipa fidia na akirudia kosa hilo atasimamishwa masomo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21) na kulipa mali iliyopotea au kuharibika***

## 9. HABARI NA MAWASILIANO

**a)** Mwasiliano ni lazima kufanyika kwa kuzingatia daraja/hadhi ya mtu unayewasiliana naye mfano kiongozi, mkufunzi, wafanyakazi wasio wakufunzi, n.k. Ni marufuku kutumia, Lugha ya matusi, dharau, kejeli, dharau au dhihaka

**b)** Msemaji mkuu na mtoa taarifa wa mambo yote ya chuo ni mkuu wa chuo. Hii ni pamoja na mialiko ya michezo, mikutano, semina, warsha baina ya wanachuo na watu wa jumuiya ya nje

**c)** Ni kosa kwa mwanachuo kutoa taarifa ya msiba, ugonjwa na taarifa zingine muhimu kutoka nyumbani zinazomuhusu mwanachuo binafsi au mwingine. Aidha taarifa ziwasilishwe ofisi ya mratibu wa masuala ya wanachuo.

**d)** Ni kosa kwa wanachuo kukusanyika au kujaribu kufanya mikutano ya aina yoyote bila ya idhini ya mkuu wa chuo

**e)** Mwanachuo au mtu yeyote yule haruhusiwi kupiga picha au kurekodi taarifa yoyote na kurusha kwa watu au katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii bila idhini ya muhusika au mkuu wa chuo

**f)** Ni kosa kwa mwanachuo kutumia simu wakati wa vipindi darasani, kwenye vyumba vya mitihani, na kwenye mikusanyiko maalumu bila maelekezo maalumu

**g)** Ni kosa kwa mwanachuo kutoa taarifa yoyote ihusuyo chuo katika vyombo vya Habari bila ruhusa maalumu kutoka kwa uongozi wa chuo

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 10(a) hadi 10(g) ataadhibiwa kwa onyo kali na kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi pia anaweza kupata adhabu zingine ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku kumi na nne (14)***

## 10. ULINZI NA USALAMA

**a)** Ni kosa kwa mwanachuo kutotii tahadhari zote za ulinzi na usalama

**b)** Ni kosa kwa mwanachuo kutotoa taarifa kwa uongozi wa chuo mara tu kunapotokea hali au tukio lisilo la kawaida

**c)** Ni marufuku kwa mwanachuo kushawishi, kuongoza, kushiriki mgomo na maandamano ya aina yoyote bila kibali

**d)** Ni kosa kwa mwanachuo kumiliki na kuishi na aina yoyote ya silaha bwenini

**e)** Ni kosa kwa mwanachuo kutoa matamshi yanayopelekea taharuki na au chuki na kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo

**f)** Ni marufuku mwanachuo kuchochea ugomvi, kugombana, kupiga, kupigana na au kuhatarisha usalama wake binafsi na au usalama wa wenzake/chuo

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 11(a) hadi 11(f) atajazishwa fomu ya onyo kali na kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi pia anaweza kupata adhabu zingine ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku ishirini na moja (21) au kuachishwa mafunzo***

**11. KAZI NA UZALENDO**

**a)** Ni kosa kwa mwanachuo kutokuheshimu, kutokuthamini na kutokujali kazi za mikono.

**b)** Ni kosa kwa mwanachuo kutokufanya kazi aliyopangiwa kwa ukamilifu na ufanisi

**c)** Kila mwanachuo lazima aoneshe moyo wa uzalendo popote atakapokuwa kwa maslahi binafsi, chuo na Taifa kwa ujumla

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 12(a) hadi 12(c) ataadhibiwa kwa onyo kali na kiongozi wa serikali ya wanachuo au mkufunzi pia atapata adhabu zingine ambazo ni usafi wa darasa, usafi wa bwalo la chakula, usafi wa choo, kubeba kifusi, kuchimba shimo la taka, kuchimba mtaro na kuotesha miti au maua. Kujirudiarudia kwa makosa haya kunaweza kupelekea mwanachuo kusimamishwa mafunzo kwa siku kumi na nne (14)***

***12.*UBAKAJI, ULAWITI NA USAGAJI/USHOGA**

a) Ni kosa kwa mwanachuo yeyote kujihusisha na vitendo vya, ubakaji, ulawiti na ushoga/usagaji.

**b)** Hairuhusiwi wanachuo wawili kulala kitanda kimoja

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 13(a)-13(b) atafukuzwa chuo au kupelekwa polisi au kutumikia adhabu zote mbili kwa pamoja***

## *13.* UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Unyanyasaji wa kijinsia au wa kimaumbile katika Chuo cha Ualimu Morogoro wa aina yoyote haukubaliki. Hii ni pamoja na;

***a)*** Kumlazimisha mtu kwa kumtaka kimapenzi kwa kutumia maneno, ishara, picha au vitisho vyenye maudhui ya kimapenzi au kumsababishia mwanachuo kukosa amani ama kushindwa kuendelea na masomo yake.

***b)*** Kutumia ishara za kufanya mapenzi katika mazingira ya Chuo au kumshikashika mtu bila ridhaa yake


***c)*** Kumkashifu au kumnyanyapaa mtu yeyote kutokana na maumbile aliyonayo au ugonjwa alionao.

***Mwanachuo atakayeenenda kinyume na sheria 14(a) hadi 14(c) ataachishwa masomo au kusimamishwa kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21)***


**Mimi……………………………………………mchepuo…………………darasa ……………………………… nimezisoma na kuzielewa sheria za Chuo cha ualimu morogoro. Naahidi kuishi kwa kuzifuata kwa muda wote nitakaokaa hapa chuoni**

**Saini……………………………………………** **Tarehe……………………………………………**

**MUONEKANO (MSHONO) WA SARE ZA CHUO KWA WANAWAKE NA WANAUME**



**SKETI** ndefu ya Heshima ivuke magoti zaidi ya inchi 5.



**SURUALI** – isiwe fupi au ya kubana. Upana wa Chini (hem) inchi 16.